**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI**

**YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule: 0693590434**

**Mwalimu Tehama: 0787630881**
**Mwandamizi Malezi: 0789246471**

**Shule ya**
**Sekondari Gehandu**

**S.L.P 172**

**MBULU-**
**MANYARA**

**Tarehe**
**.................……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**…………………………………………….**
**…………………………………………**
**S.L.P …………………………….…**
**…………………………………………….**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI GEHANDU HALMASHAURI YA MJI WA MBULU MKOA WA MANYARA MWAKA ……………**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka………………… **na atasoma tahasusi ya………………..** Shule ya Sekondari Gehandu ipo katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu Mkoa wa Manyara umbali wa Kilometa 08 kutoka Mbulu mjini. Usafiri wa kutoka Mbulu mjini hadi shuleni unapatikana katika kituo cha mabasi Mbulu**.** Nauli ni Shilingi **1000** Kwa daladala na shilingi **3000** kwa pikipiki na Shilingi **5000** kwa bajaji.

**Muhula wa Masomo unaanza tarehe …………………hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe……………Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………**

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:**

2.1 **Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni **Sketi mbili** kwa Wasichana na **Suruali mbili** kwa Wavulana yenye rangi ya **DARK GREY (Kijivu Kilichokolea) namba moja**.

a. Sketi iwe na mshono wa mstari mkubwa mbele na nyuma na mistari midogo miwili kila upande wa nyuma na mbele na iwe na zipu na kifungo upande wa kushoto. Sketi iwe ndefu chini ya magoti, kutoka kwenye goti isipungue sentimita 30.

b. Kwa wavulana suruali iwe na sereblesheni, misuko miwili mbele na mfuko mmoja nyuma upande wa kulia.

ii. Mashati mawili meupe ya Tetron yenye mikono mirefu.

iii. Rangi ya Hijab (Kijuba) ni **Nyeupe** ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Sare ya Michezo ni jezi **MOJA** ya **DARK BLUE** na Raba Jozi moja Kwa wasichana na jezi moja ya **DARK BLUE** na raba Jozi **MOJA** kwa wavulana.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi kwa wavulana na wasichana.

vi. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi jozi mbili kwa wavulana.

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali kwa wavulana.

viii. Sweta moja yenye rangi ya **DARK GREY** yenye shingo ya **V** kwa mbele.

ix. Tai ya rangi ya **Dark Grey** kwa wote.

x. Pull neck ya **Dark Grey** au **Nyeupe** kwa ajili ya baridi

xi. **Mwanafunzi aje na Tisheti moja yenye rangi ya Dark Blue yenye Kola isiyo na Maandishi wala picha au kama mzazi atashindwa kuipata ataikuta shuleni kwa bei ya Tsh.15,000.**

2.2 **Nguo za Kushindia**

- **Wasichana**:Sketi mbili za rangi **Nyeusi** namba moja mshono ufanane na sketi ya shule.
- **Ushungi wa Dark Blue** kwa Wanafunzi wa Kike Waislamu. Ataiva baada ya masomo na siku za weekend.
- **Wavulana:** Suruali mbili za rangi **Nyeusi** namba moja, mshono ufanane na Suruali ya Shule.

2.3 **Mahitaji Mengine Muhimu ambayo Mwanafunzi anapaswa kuja nayo Shuleni:**

i. Madaftari **QUIRE 4** yasiyopungua **08**

ii. **RIMU MBILI (02) A4**.

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi yetu imeambatishwa nyuma ya fomu hii ya maelekezo.

iv. Scientific Calculator.

v. Mathematical set, kalamu za wino na risasi za kutosha, ufutio na rula.

vi. Godoro la sponji urefu futi sita, upana futi 2½ una unene inchi Tatu (3).

vii. Lab coat nyeupe kwa ajili masomo kwa vitendo

viii. Mashuka Jozi 2 za rangi ya kijani, blanket 1, foronya ya godoro 1 rangi ya kijani na chandarua nyeupe 1.

x. Nguo za ndani za kutosha na taulo za kike za kutosha kwa wasichana

xi. Tracksuit moja (1) rangi ya Dark blue yenye mistari meupe

xii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

xiii. Ndoo 2 kubwa (lita 20) zenye mifuniko;

xiv. **Vifaa vya usafi:** Wavulana waje na Mopa 1, Hard Broom1, Ufagio wa chelewa 1, na Jembe 1 lenye mpini. Wasichana waje Mopa 1, Soft Broom 1, Ufagio wa chelewa 1, na slesha 1.

xv. Aje na Tochi moja iwe na betri kwa ajili ya tahadhari pindi umeme unapokatika.

xvi. Vyombo vya chakula (Sahani, Bakuli, Kijiko na Kikombe) vya aluminium. Vyombo vya Plastiki haviruhusiwi shuleni.

xvii. **Sanduku la Bati (Tranka) imara la kufunga kwa kofuli.**

xviii. Sabuni ya maji ya kufanyia usafi chooni lita tano.

xix. Aje na **KOPI** ya Result Slip au Cheti cha CSEE 2025 na **KOPI** ya Leaving Certificate wakati wa kuripoti Shuleni. Nakala mbili

## 2.4 Michango Mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** Fedha hizo zilipwe kwenye Account ya Shule **Na.41202300528** katika Benki ya **NMB** Tawi lolote. Jina la Account: **GEHANDU SECONDARY SCHOOL GENERAL FUND ACCOUNT** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye **Pay in slip** na mwanafunzi aje nayo na kuikabidhi ofisi ya fedha mara afikapo shuleni).

**TANBIHI: Kwa kuwa ghrama za matibabu zimekuwa kubwa** kila mwanafunzi anapaswa kuja na **Bima ya Afya ya NHIF** na kukabidhi ofisi ya Mkuu wa Shule mara afikapo shuleni. Kama hana Bima ya Afya ya NHIF aje na **Tsh.50,400/=** ili apatiwe Bima ya NHIF yenye kumudu gharama za matibabu.

**Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 2.5 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ✞ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- ✞ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**
- ✞ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**2.6 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

3. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

    i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
    ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
    iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
    iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4. ***Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

***Saini na Muhuri wa Mkuu wa Shule…………………***

***Jina la Mkuu wa Shule…………………***

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA
ZIFUATAZO:**

- ➢ **Mkuu wa Shule: 0694452545**
- ➢ **Mwalimu Tehama: 0787630881**
- ➢ **Mwandamizi Taaluma 0786301092**
- ➢ **Mwandamizi Malezi 0789246471**

**FOMU A**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI GEHANDU,**
**S.L.P 172,**
**MBULU.**

**HATI YA MAKUBALIANO**

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………….
ANWANI……………………….........................................................................

TAREHE…………………………………………………………………….
KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE YA SEKONDARI GEHANDU

Mimi ……………………………………….. kidato cha ……………. Ninayakubali masharti na kuwa nitatii sheria za Shule zilizoko na zile zitakazotolewa kwa muda wote wa masomo yangu. Naahidi kuwa nitawaheshimu na kuwatii walimu wote wa shule na wafanyakazi kama walezi wangu na wanafunzi wenzangu.

Naahidi kuwa nitatii wale wote watakaoteuliwa au kuchaguliwa kuwa viongozi wangu kwa mujibu wa sheria

Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mwaminifu. Naahidi pia kuwa nitajielimisha kwa nguvu zangu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu.

Natambua kuwa nikikiuka ahadi hizi nitapoteza nafasi yangu ya kuwa mwanafunzi hapa shuleni.

**JINA LA MWANAFUNZI ………………………………………………**

**SAINI YA MWANAFUNZI……………………………………………**

**JINA LA MZAZI/MLEZI ……………………………………………...**

**SAINI YA MZAZI/MLEZI…………………………………………….**

**Anuani ya Mzazi/Mlezi…………………………………………….**
**Namba ya simu ……………………………………………….**

**<u>FOMU B</u>**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**THE PRIME MINISTER'S OFFICE**

**GEHANDU SECONDARY SCHOOL**

**P.O.BOX 172**

## MEDICAL FORM

To be completed by medical officer from a recognized Government Hospital.

Full Name of Student…………………………………………………………….

Sex: Male ( ) Female ( )

Blood count (Red and White) ………………………………………………….

Stool examinations …………………………………………………………….

Sexually Transmitted diseases………………………………………………….

T.B ………………………………………. Skin………………………….

Eye test……………………………………. Ears………………………………

Chest………………………………………. Spleen………………………………

Abdomen………………………………Pregnancy………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION**

E.g Physical defects/impairment pediatric disorders……………………...........

I certify that the above-named Student is fit/unfit to pursue her/his studies as stated above.

Name ……………………………………Signature………………Title………………….

**MEDICAL OFFICER**

DATE……………………………. Stamp……………………………………………

NOTE: Student should send or bring the completed form to school.

**FOMU C**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU -TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI GEHANDU**
**S.L.P 172,**
**MBULU**
.

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. **ANDIKA MAJINA KAMILI**

| Jina la kwanza | Jina la pili | Jina la tatu | Umri | Tarehe ya Kuzaliwa |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**2. MAHALI UNAKOTOKA**

a. Kijiji / Mtaa ……………………Kata.......................................................................................
Tarafa ……………………. Wilaya………………………. Mkoa…………………………

b. Anwani ya nyumbani…………………………………. SIMU………………………..….

c. Kukiwa na matatizo taarifa ipelekwe kwa **(JINA)**……………………………………….
Uhusiano na wewe……………………………………………………………………………
Anafanya kazi gani…………………………. Na wapi……………………………………….

d. Dini yako……………………. Dhehebu……………………...

e. Unaishi na nani na wapi(jina)..................................na (mahali)……………Namba yake ya Simu…………………Nani anayekupa mahitaji ya shule……………………………………. namba yake ya simu…………………………
Toa sababu kama siyo mzazi.........................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................

## <u>ORODHA YA VITABU VYA MASOMO</u>

**Mzazi unaweza ukamnunulia mwanao vitabu vifuatavyo**

### CHEMISTRY

1. Physical Chemistry, by Delungu (Mzumbe Bookshop Project 1998)
2. Advanced inorganic Chemistry part I and II (Tanzania Institute of Education)
3. Organic Chemistry part I, The fundamental Priciples I.L Finar (LongmanLTD)
4. Physical Chemistry by Ngaiza

### GEOGRAPHY

5.The newest practical geography alive, 2024 Edition. by TIE (Tanzania Institute of Education)

6.The newest physical geography alive, 2024 Edition by TIE (of Tanzania Institute Education)

### BIOLOGY

11. Biological science; Cambridge university press 1997 3rd edition
12. New understanding biology by Suzan Toole
13. Advanced biology by Michael Kent (2000). Oxford university press Uk.
14. Biology for Secondary Schools student's book Form Five: Advance Biology Principles and Application by C J Clegg and Mackean.

### BASIC APPLIED MATHEMATICS

15. Basic applied Mathematics by Kiza and Septine I Sillem
16. Historia ya Tanzania na Maadili Kidato Cha Tano


### KISWAHILI

17. Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi kidado cha Tano 2024: Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE).
18. Umahiri Katika Nadharia ya Lugha Kiswahili 1 2023: Chacha S.M.
19. Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili 2023: Chacha S.M.
20. Fasihi ya Kiswahili Kwa Shule za Sekondari – Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha TIE
21. Dunia Uwanja Wa Fujo (2023)-Euphrase Kezilabi: Africa Proper Education Network
22. Ua La Faraja (2007) -W.E. Mkufya: Mangrove Publishers
23. Mirathi Ya Hatari (2023) -C. G. Mung'ong'o: Mkuki na Nyota Publishers Ltd
24. Wasifu wa Siti Binti Saad (2023)- Shaaban Robert:Mkuki na Nyota Publishers Ltd
25. Mukwava wa Uhehe (2023)- M. M. Mulokozi: Africa Proper Education Network
26. Shujaa Mirambo (2023)-Emmanuel Mbogo: Africa Proper Education Network
27. Usaliti Mjini (2024)-Francis Imbuga: East Africa Educational Publishers Ltd


28. Fumbo Linaloelea (2023)-Nyambari .C.M.Nyangwine: Mbesa Books Distributors
29. Malenga wa Ziwa Kuu (2024)-Wallah Bin Wallah: East Africa Educational Publishers Ltd
30. Andamo, Msafiri Safarini (2023)-Mohamed Khelef Ghassani: Educational Books Publishers Ltd
31. Wosia wa Baba (2024)-Ahmed Mohamed Amanzy: Abantu Publications Ltd
32. Vuta N'kuvute(2007)-Shafi Adam Shafi: Mkuki na Nyota Publishers Ltd
33. Asali Chungu (2024) Said Ahmed Mohamed: East African Educational Publishers Ltd
34. Mwana wa Yungi Hulewa(2023)- Mohammed Said Abdulla: East African Educational Publishers Ltd
35. Vipuli vya Figo (2024)- Emmanuel Mbogo: East African Educational Publishers Ltd
36. Kaptula la Marx (2023)-Euphrase Kezilahabi: Africa Proper Education Network
37. Nyerere na Safari ya Kanaani (2023)- Emmanuel Mbogo: Africa Proper Education Network
38. Morani (2007)-Emmanuel Mboga: Africa Proper Education Network
39. Dhifa (2023)- Euphrase Kezilahabi: Africa Proper Education Network
40. Utenzi Majumui wa Karne ya 21(2023) Iddi M.Mwimbe: Nyambari Nyangwine Publishers
41. Malenga wa Bara (2023)-M.M Mulokozi na K.K Kahigi: African Proper Education Network
42. Fungate ya Uhuru (2007)-Mohammed Seif Khatibu: Africa Proper Education Network

**HISTORI YA TANZANIA NA MAADILI**

43. Historia ya Tanzania na Maadili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato Cha Tano (2024) Taasisi ya Elimu Tanzania



**UNIFORM KWA AJILI YA WASICHANA NA MISHONO YAO**



**UNIFORM KWA AJILI YA WAVULANA NA MSHONO WAKE**